## Muozo biri (Cigar end rot)

### Utangulizi

Muozo biri ni ugonjwa muhimu wa migomba ambao husababishwa na kuvu ajulikanaye kwa jina la Verticillium theobromae. Ugonjwa huu huenea zaidi kwenye mashamba mengi ya migomba. Hushambulia vidole vya ndizi, vidole hukauka na kufanana na rangi ya kijivu kama majivu ya sigara. Mkungu wa ndizi ulioshambuliwa na ugonjwa huu hupunguza ubora na thamani yake. Ugonjwa huu husambaa zaidi wakati wa joto.

### Dalili za uharibifu

- Ncha ya vidole vya ndizi huoza na kufunikwa na ukungu wa kijivujivu hatimaye hufe.
- Madoa meusi hujitokeza kwenye ganda mithili ya kashata ambayo huishia kufunika mkungu wote.





### Udhibiti

- Ondoa majani makavu yanayoning'nia, fumb fumbu, ua dume ambalo ukungu huanzia ili kuruhusu mzunguko wa hewa shambani.
- Teketeza mikungu na mashina yaliyoathirika kuondoa chanzo cha maradhi.
- Pogolea migomba ili kuipunguza kubakiza yenye afya ukifuata umri (mama, dada, mjukuu na kitukuu).
- Ugonjwa ukizidi shambani nyunyizia mchanganyiko wa magadi soda gramu 100 na sabuni ya unga gramu 50 kwenye lita 2 za maji.
- Nyunyizia kiuatilifu aina ya Indofil M 45 (0.25 %) kwenye majani au Bavistin (0.05 %) kwenye mikungu ya ndizi.



Ugonjwa wa mnyauko fusari kwenye jani la mgomba



Ugonjwa wa sigatoka nyeusi kwenye jani la mgomba


PIGA SIMU BURE:
**080 011 003 1**

P.O. Box 3024 , Arusha - Tanzania Nairobi Rd, Ngaramtoni Area

**Phone** +255 739 970 467
**Web** www.tphpa.go.tz
**Email** dg@tphpa.go.tz

tphpa_tz  tphpa_tz  TPHPA HABARI TV

SCAN FOR MORE


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KILIMO

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA



# UDHIBITI HUSISHI WA VISUMBUFU VYA MIGOMBA

## Bungua wa migomba

**(Banana weevil)**

### Utangulizi

Bungua wa migomba ni mdudu hatari sana kwenye zao la migomba. Bungua huishi kwenye mabaki ya mimea ya migomba na kwenye udongo.

### Dalili za uharibifu

- Bungua hushambulia tunguu la migomba na kuacha vishimo ambayo hunyima mgomba uwezo wakusafirishha chakula na maji toka ardhini

- Migomba iliyoathiriwa huanguka chini wakati wa mvua na upepo mkali.





### Udhibiti

- Chonga mizizi ya machipukizi yanayotumiwa kama mbegu sehemu ya nje ya tunguu la mgomba kisha tumbukiza miche iliyochon wa kwenye maji yaliyochemshwa nyuzi joto 100 kwa sekunde 30 kuua funza wa bungua.

- Baada ya kuvuna mikungu ya ndizi, chimbua tunguu kisha katakata vipade vidogo vidogo, sambaza yakauke kuua mazalia ya funza wa bungua.

- Weka unga wa muarobaini gramu 60-100 kwenye shina la mgomba wakati wa kupanda na kila baada ya miezi 4 kuua bungua

- Weka matandazao shambani kuhifadhi uyevunyevu na kuzuia uotaji wa magugu

## Wadudu mafuta

**(Banana Aphids)**

### Utangulizi

Mdudu mafuta kamili ana maumbile mbali mbali; wadogo sana,wa kati na wakubwa kiasi, ni wangavu, wenye rangi nyekundu na weusi. Wadudu hawa ni hatari kwa zao la migomba kwani husambaza ugonjwa wa mkungu ambao umeripotiwa nchini Hawii.

### Dalili za uharibifu

Machipukizi ya migomba hushambuliwa zaidi na mdudu mafuta. Mashambulizi yake husababisha mmea kulemaa, majani kujikunja na kukakamaa, hatimae mmea hutengeneza vifundo kwenye majani





### Udhibiti

- Hakikisha shamba ni safi kila wakati kwa kuondoa magugu, kupunguza majani ya migomba, na machipukizi.

- Nyunyiza kiuadudu Attakan 350 SC au Confidor 200 SL kwenye migomba kulingana na maelekezo yaliyoko kwenye kiambatanisho kilichopo kwenye kifungashio cha kiuadudu husika.

- Pata ushauri kutoka kwa afisa ugani wa eneo lako.

## Vithiripi wa migomba

**(BananaThrips)**

### Utangulizi

Vithiripi wa migomba ni wadudu wadogo, wembamba, warefu, weusi wa kung'ara ambao huonekana kwenye chane hasa sehemu ya mwisho ya ua la ndizi. Vithiripi kamili hutaga mayai chini ya ndizi (tunda) changa na kishika matunda ya ndizi.

### Dalili za uharibifu

Sehemu ya mmea iliyoshambuliwa huwa na mabaka ya rangi ya fedha na nta. Mashambulizi yakizidi mabaka hugeuka kuwa na rangi nyekundu kahawia, pamoja na mikwaruzo na nyufa zinazoonekana kwenye ngozi ya tunda la ndizi.





### Udhibiti

- Kagua shamba mara kwa mara kubaini uwepo wa vithiripi baada ya kukagua weka witego ya bluu 4-5 kwa ekari kunasa vithiripi.

- Kusanya na kuchoma moto majani, mmea na m tunda yaliyoshambuliwa na vithiripi wa migomba

- TPalilia shamba la migomba kila magugu yanaoa za kuota ili kuzuia vithiripi kujihifadhi wakati wa baridi.

## Wadudu mafuta

**(Banana Aphids)**

### Utangulizi

Mdudu mafuta kamili ana maumbile mbali mbali; wadogo sana,wa kati na wakubwa kiasi, ni wangavu, wenye rangi nyekundu na weusi. Wadudu hawa ni hatari kwa zao la migomba kwani husambaza ugonjwa wa mkungu ambao umeripotiwa nchini Hawii.

### Dalili za uharibifu

Machipukizi ya migomba hushambuliwa zaidi na mdudu mafuta. Mashambulizi yake husababisha mmea kulemaa, majani kujikunja na kukakamaa, hatimae mmea hutengeneza vifundo kwenye majani





### Udhibiti

- Hakikisha shamba ni safi kila wakati kwa kuondoa magugu, kupunguza majani ya migomba, na machipukizi

- Nyunyiza kiuadudu Attakan 350 SC au Confidor 200 SL kwenye migomba kulingana na maelekezo yaliyoko kwenye kiambatanisho kilichopo kwenye kifungashio cha kiuadudu husika.

- Pata ushauri kutoka kwa afisa ugani wa eneo lako.